# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

# BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO

## LINDI RVTSC

## 2025


Simu: 0232935150

P.O. BOX 1001, LINDI

Nukushi: 0732933370

lindirvtsc@veta.go.tz

www.veta.go.tz


Kumb. Na;

4/12/2024

Ndugu

______________________________

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA LINDI RVTSC Mwaka 2025

MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika

   Fani ya ______________________

   Katika ngazi Level One

   mwaka wa I ______________
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 13/01/2025
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Fedha ikishalipwa hairudishwi. Kama fedha za tahadhali (caution Money) hazikutumika zitarudishwa
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo k

ma utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo

______________________________

Harry Mmari

MKUU WA CHUO

**MAELEKEZO KWA WANACHUO.**

1. Utatakiwa kuzingatia vipindi vyote vya masomo vikiwemo vya nadharia na vitendo. Uongozi wa chuo unaweza kuchukua uamuzi wa kukusimamisha kuendelea na mafunzo katika kipindi cha miezi mitatu, iwapo itathibitika kuwa uwezo wako kimasomo ni mdogo.
2. Ada ya mafunzo ni Tshs. **60,000/=** kwa mwaka kwa wanafunzi wa kutwa na Tshs. **120,000/=** kwa mwaka kwa wanafunzi wa Bweni malipo yote yafanyike **kupitia namba "control number" uliyopewa** chuoni siku ya kuchukua fomu ya maelezo ya kujiunga na chuo namba hii utaiwasilisha benki wakati wa kulipia ada na michango yako ya mwaka (ada hizi zinaweza kubadilika wakati wowote na mtapewa taarifa ikitokea hivyo)

   Malipo ya ada pekee yanaweza kufanyika kwa awamu mbili muhula wa kwanza na muhula wa pili,michango mingine yote ifanyike muhula wa kwanza **(ada ya mitihani wa taifa italipwa muhula wa pili baada ya kupewa Control Number kutoka Ofisi ya Kanda)**
3. Wakati wa kusajiliwa mwanafunzi anatakiwa afike na stakabadhi ya malipo ya ada na michango mengine kutoka benki (Bank pay in slip) vivuli (Nakala) ya vyeti, picha nne 4 (passportsize) za hivi karibuni na fomu ya uthibitisho wa afya yako kutoka kwa daktari wa hospitali ya serikali.

4. **Mwanafunzi atapaswa kuja na vifaa vifuatavyo siku ya kuripoti chuoni:**

 i. Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya tetroni.
 ii. Shati moja jeupe la mikono mirefu kwa wanafunzi wa FBSS tu.
 iii. Jozi ya viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kufunga na kamba na visiwe aina ya "moccasin" au "four angles"
 iv. Buti za usalama rangi nyeusi zenye Chuma mbele kwa fani za WF,CJ,RAC,MB,MVM,EL, PPF
 v. Tape measure (Kwa fani za CJ, WF na PPF tu).
 vi. Vifaa vya hesabu (Mathematical set).
 vii. Daftari 8.
 viii. Drawing pencils (Penseli za kuchorea).
 ix. Karatasi nyeupe **(Photocopy paper)** Rimu moja A4 kwa wanafunzi wote
 x. Karatasi ya mistari **(Ruled paper)** Rimu moja kwa wanafunzi wote.
 xi. Jembe 1 na mpini kwa fani za WF, DSCT, BOA
 xii. Sururu 1 na Mpini kwa fani ya PPF na MB
 xiii. Sepetu (Chepe) 1 kwa fani ya LAB
 xiv. Kwanja 1 kwa fani za EL, RAC na MVM.
 xv. Panga 1 kwa fani za CJ, BOA, FBSS na FP
 xvi. **Wanafunzi wa Bweni** wafike na Vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi binafsi mto 1 pamoja na foronya 2, shuka 2, taulo 1, soksi jozi 4, Chandarua 1, Bakuli 1, Sahani 1, Kikombe 1 na Kijiko, Ndoo ndogo 1, Kandambili, Sabuni ya kuogea na kufulia, Dawa ya meno, mavazi na vifaa vingine muhimu kwa ajili ya usafi binafsi.

**5.** Malipo kwa ajili ya Vifaa/huduma vinavyopatikana chuoni yafanyike **kupitia namba “control number” uliyopewa** siku ya kuchukua fomu ya maelezo ya kujiunga. Vifaa hivyo ni kama ifuatavyo:

i. Fulana(tisheti) moja
ii. Suruali mbili za bluu
iii. Ovaroli moja khaki rangi ya bluu kwa fani za WF,CJ,RAC,MB,MVM,EL
iv. Overcoat moja rangi nyeupe kwa fani ya DSCT na Maabara (LAB)
v. Mavazi maalum kwa fani ya za FP na FBSS
vi. Nembo za VETA
vii. Fedha za tahadhari (caution money) kwa mali za Chuo
viii. Mchango kwa ajili ya michezo
ix. Chai ya asubuhi kwa wanafunzi wa kutwa
x. Bima ya afya NHIF (kwa wasionayo)
xi. Gharama ya kukodi godoro kwa mwaka (Kwa wanafunzi wa bweni tu)
xii. Gharama ya Kitambulisho
xiii. Gharama za shughuli za mahafali
xiv. Mchango kwa ajili ya serikali ya wanafunzi
xv. Ada ya mtihani wa Taifa ambayo italipwa katika muhula wa pili baada ya mwanafunzi kujisajili kufanya mtihani.

**NB: Gharama kwa ajili ya** Vifaa vilivyoorodheshwa hapo juu zimechanganuliwa vizuri kwenye majedwali hapo chini:

| **MCHANGANUO WA ADA NA MICHANGO MINGINE KWA MWAKA 2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **WANAFUNZI WA BWENI** | | | | |
| | **WF,CJ,RAC,MB,MVM,EL, PPF** | **DSCT, LAB** | **FP, FBSS** | **SC, BOA** |
| ADA YA MAFUNZO MUHULA I | 60,000 | 60,000 | 60,000 | 60,000 |
| GODORO | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| MICHEZO | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| BIMA YA AFYA | 50,400 | 50,400 | 50,400 | 50,400 |
| SEKIKALI YA WANAFUNZI | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 |
| NEMBO YA VETA | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| SURUALI 2 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| OVERALL(NGUO ZA KAZI) | 40,000 | 35,000 | 90,000 | - |
| TISHETI | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| KITAMBULISHO CHA CHUO | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| FEDHA YA TAHADHARI (CAUTION) | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| MAHAFALI | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| **JUMLA MICHANGO MINGINE** | **297,400** | **292,400** | **347,400** | **257,400** |
| **JUMLA KUU MUHULA WA KWANZA** | **357,400** | **352,400** | **407,400** | **317,400** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ADA YA MTIHANI | 25,000 | 25,000 | 30,000 | 30,000 |
| ADA YA MAFUNZO MUHULA II | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| **JUMLA KUU MWAKA MZIMA** | **352,400** | **347,400** | **407,400** | **317,400** |
| | | | | |
| | | | | |
| **MCHANGANUO WA ADA NA MICHANGO MINGINE KWA MWAKA 2025** | | | | |
| **WANAFUNZI WA KUTWA** | | | | |
| | **WF,CJ,RAC,MB,MVM,EL, PPF** | **DSCT, LAB** | **FP, FBSS** | **SC, BOA** |
| ADA YA MAFUNZO MUHULA I | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| CHAI | 25,000 | 25,000 | 25,000 | 25,000 |
| MICHEZO | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| BIMA YA AFYA | 50,400 | 50,400 | 50,400 | 50,400 |
| SEKIKALI YA WANAFUNZI | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 |
| NEMBO YA VETA | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| SURUALI 2 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| OVERALL(NGUO ZA KAZI) | 40,000 | 35,000 | 90,000 | - |
| TISHETI | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| KITAMBULISHO CHA CHUO | 5,000 | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| FEDHA YA TAHADHARI (CAUTION) | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| MAHAFALI | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| **JUMLA MICHANGO MINGINE** | **267,400** | **262,400** | **317,400** | **227,400** |
| **JUMLA KUU MUHULA WA KWANZA** | **297,400** | **292,400** | **347,400** | **257,400** |
| ADA YA MTIHANI | 25,000 | 25,000 | 30,000 | 30,000 |
| ADA YA MAFUNZO MUHULA II | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| **JUMLA KUU MWAKA MZIMA** | **322,400** | **317,400** | **377,400** | **287,400** |

Kielelezo:
**EL-** Umeme, **RAC-** Viyoyozi na Majokofu, **MVM-** Magari, **WF-** Uchomeaji na Uungaji vyuma, **CJ-** Useremala, **MB-** Uashi, **PPF-** Ufundi bomba, **SC-** Uhazili, **BOA-** Biashara, **FBSS-** Uhudumu wa Hoteli na Vinywaji, **FP-** Upishi, **DSCT-** Ushonaji na Ubunifu wa Nguo, **LAB-** Maabara

6. Mwanachuo hatapokelewa Chuoni iwapo atafika bila kutekeleza vipengele vilivyotajwa hapo juu.
7. Ada ikishalipwa haitarudishwa. Endapo fedha ya tahadhari (caution money) haitatumika katika kipindi chote mwanafunzi awapo chuoni, fedha hiyo atarejeshewa mwanafunzi amalizapo masomo.
8. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za Chuo kama zilivyoambatanishwa kwenye barua hii.
9. Nafasi yako kama mwanachuo itapotea endapo utashindwa kuripoti Chuoni **wiki mbili** zaidi baada ya tarehe ya kufungua chuo.
10. Fika na barua hii siku ya kuripoti Chuoni

**Muhimu:** mwanafunzi hatopokelewa chuoni iwapo hatakamilisha malipo ya muhula wa kwanza kama ilivyooneshwa kwenye majedwali yaliyoambatishwa.

Uongozi wa Chuo unakupongeza kwa kupata nafasi hii.

**KARIBU CHUO CHA VETA- LINDI**

**TARATIBU NA SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI**

**Katika kipindi chote mwanafunzi awapo chuoni atatakiwa kuzingatia sheria na taratibu zifuatazo.**

**MUHIMU**

(a) Kila mwanafunzi anapaswa kuwa katika eneo la chuo kabla au ifikapo saa 1.30 asubuhi.

(b) Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya chuo kwa sababu yoyote ile bila ruhusa ya Mwalimu wa zamu. Atayebainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo na kugharamia uharibifu uliojitokeza kutokana na kutoroka kwake.

(c) Ruhusa ya kumlazimu mwanafunzi kulala nje ya chuo, ipitishwe, kwa mwalimu mlezi (matron /Patron) na Mwalimu wa zamu kabla ya kufikishwa kwa Msajili..

(d) Mahudhurio chini ya 85% yatamsababishia mwanafunzi kukosa cheti cha kumaliza mafunzo (leaving certificate).

(e) Mwanafunzi hatoruhusiwa kuendelea na mafunzo iwapo hatofikisha wastani wa alama 60 katika kila somo linalofundishwa chuoni.

(f) Iwapo mwanafunzi ataonesha udhaifu katika masomo ndani ya miezi mitatu ya mwanzo atasimamishwa kuendelea na masomo mara moja.

(g) Mwanafunzi hatasajiliwa kufanya mtihani wa mwisho (CBA) akishindwa kufikisha wastani wa alama 60 kwenye somo lolote.

**1. MAVAZI**

(a) Sare ya Chuo ni suruali ya rangi ya Bluu na shati jeupe la mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni, wakati wa kuja Chuoni na kurudi nyumbani kwa wanafunzi wa kutwa na siku za mapumziko kwa wanafunzi wa Bweni na Hosteli wanapotoka nje ya chuo. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

(b) Ovaroli/nguo za kazi livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Wanafunzi wa kike watakaovaa hijabu inapaswa isivuke mfuko wa shati ili nembo ya chuo ionekane vizuri.

(d) Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au sandozi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

**2. USAFI WA MWILI**

a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote kwa kipindi chote cha mwanafunzi awapo chuoni.

b) Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali

**c) Nywele kwa wavulana**

- Zikatwe ziwe fupi na mitindo kama “PANKY”, “AMERICAN BASE” NA KIPARA hairuhusiwi kabisa.
- Ndevu haziruhusiwi.

**d) Nywele kwa wasichana**

- Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mstari (twende kilioni)

NB: Nywele ndefu na nywele zenye kupakwa madawa kama vile “carl”, “raster” na “golden hair” haziruhusiwi kabisa kwa kipindi chote cha mafunzo.

**3. WIZI**

(a) Wizi au vitendo vyovyote vinavyo husishwa na wizi haviruhusiwi, endapo itathibitika kuwa mwanafunzi ameiba au kuhusishwa katika tukio lolote la wizi adhabu yake ni kufukuzwa chuo.

(b) Ukipoteza vifaa vya Chuo utatakiwa kulipa au kufidia gharama kamili ya kifaa kilichpotea ndani ya majuma mawili.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya karakana za chuo.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na wakati wa kutoka getini

**4. UGOMVI**

Ugomvi, kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Mwanachuo atakayepatikana akijihusisha na vitendo vya nanma hiyo atafukuzwa Chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.

**5. ULEVI:**

Iwapo itathibitika kuwa Mwanafunzi analewa, au kuonekana katika sehemu za vileo anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa Chuo mara moja.

**6. MAPENZI**

(a) Uhusiano wa kimapenzi Chuoni kati ya Mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.

(b) Mwanachuo akipata mimba hataruhusiwa kuendelea na masomo akiwa kwenye hali hiyo.

**7. MIGOMO:**

Migomo au kuchochea migomo ni kosa kwa mujibu wa taratibu na sheria za chuo hiki. Mwanachuo atakayeshawishi, kusababisha au kushiriki migomo atafukuzwa Chuo.

**8. LUGHA**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni Kiingereza hivyo ni wajibu wa kila Mwanafunzi kujifunza Kiingereza.

**9. KUBADILI JINA**

Mwanafunzi hataruhusiwa kubadili Jina ispokuwa pale itkapothibitika kuwa ni lazima kufanya hivyo, kwa uthibitisho wa kisheria.

**ONGEZEKO LA SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI:**

Wanachuo wa bweni wataamka saa kumi nambili asubuhi na kufanya usafi wa mazingira wanamoishi**.**

10. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo:

(i) Jumamosi tangu saa 4:30 asubuhi hadi saa 11:00 jioni.
(ii) Jumapili tangu saa 12:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni.
(iii) Siku za sikukuu saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni

Hairuhusiwi kutoka nje ya Chuo wakati mwingine wowote bila kibali maalum.

11. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuvaa sare ya Chuo yenye nembo ya VETA. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuvaa sare yenye nembo ya VETA atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa Chuoni.

12. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya Chuo bila kubali atafukuzwa chuo na kugharamia uharibifu wowote uliotokana na kosa hilo.

13. Hairuhusiwi kupika wala kupeleka chakula bwenini, endapo kuna mgonjwa ruhusa itatolewa na Mwalimu wa zamu/mlezi wa bweni. Atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua za kinidhamu.

14. (a) Ni marufuku Wanachuo wa Kiume na Wakike kutembeleana mabwenini.
(b) Hairuhusiwi KABISA kwa mwanachuo kuingia katika makazi ya wafanyakazi wa Chuo bila ya ruhusa ..

15. Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:30 za usiku.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha au kumlaza mgeni bwenini.
(a) Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 11:00 jioni.
(b) Kila Jumapili na siku za Sikukuu kuanzia saa 1:00 asubuhi mpaka 11:00 jioni.

17. Vyumba/Madarasa na vifaa vingine vitumiwe kwa kadiri ya matumizi yaliyokusudiwa . Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

18. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya Chuo itatolewa na ofisi ya Mkuu wa Chuo.

19. Ruhusa ya kutoka Chuoni, Jumamosi saa 4:00 asubuhi hadi saa 11.00 jioni. Jumapili na siku za Sikukuu saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. Majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mwanachuo atapaswa kuandika katika daftari la walinzi getini muda wa kutoka na kusaini arudipo

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY**

**LINDI REGIONAL VOCATIONAL TRAINING AND SERVICE CENTRE**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Admission to LINDI RVTSC is conditional upon receipt of satisfactory medical report. The practitioner to whom this form is presented is requested to examine the candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an………………................... (Trade)

The Medical Officer

…………………………….

…………………………….

…………………………….

…………………………….

Please examine ……………………………………………. (Candidates name)

(i) Eyesight……………………………………………

(ii) Hearing…………………………………………….

(iii) Height……………………………………………..

(iv) Allergies……………………………………………

(v) Weight…………………………………………….

(vi) Asthma…………………………………………….

(vii) Epilepsy……………………………………………

(viii) Other serious diseases……………………………..

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that/she is physically fit/unfit for training as above.

**TITLE………………………………………SIGNATURE…………………..**

**Official Stamp……………………………… Date…………………………….**

AFFIX YOUR
PASSPORT SIZE
HERE

**TAARIFA YA MWANACHUO (PERSNAL PARTICULARS)**

**Part (A)**

To be completed by the student (use block letters)

1. Last name MR/MRS/MISS……………………………………………

2. Other names……………………………………………………………

3. Place of birth (District)…………………………….Village/town….......

4.Education level…............Name of school studied.........................................................

5. Occupation Selected …..................................................

6. Date and year of birth………………………………………………….

7. Marital status………………………(single/married)

8. Permanent home address……………………………………………..

9. Name of Guardian/Parent………………………………………………

10. Postal address………………………………………………………...

11. Mobile phone………………………………………………………….

**Declaration**

I …………………………………………………hereby certify that, I accept this offer, and that the foregoing information, I have given is correct to the best of my knowledge. Signature………………………. Date………………

**Part (B)**

Ijazwe na Mzazi/Mlezi/Mdhamini

Mimi ………………………………….. S.L.P. …………………………………………

Simu ya mkononi………………………

Ninathibitisha kuwa ninamdhamini mtajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za Mafunzo (ada) n.k. pamoja na nauli wakati wote wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo ya awali.

**Tarehe………………. Sahihi………………………..Uhusiano……………………………………………**